# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA SITA

**15 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 15 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**69. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kujenga majengo katika Kituo cha Afya Kazuramimba - Uvinza.

**70. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza na kumaliza ujenzi wa Stendi ya kisasa ya Jiji la Arusha katika eneo la *Bondeni City.*

**71. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika kuhakikisha fursa zote za mikopo zinatolewa kwa uwiano unaozingatia usawa katika Halmashauri zote.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**72. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Serikali itawalipa Wastaafu waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjwa Mwaka 1977.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**73. MHESHIMIWA ABDI HIJA MKASHA (MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Kamera zilizofungwa Mji Mkongwe - Zanzibar zinasaidiaje katika kupambana na kudhibiti uhalifu kwenye maeneo hayo.

**WIZARA YA UJENZI:**

**74. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, nini mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kiranjeranje - Nanjirinji - Ruangwa kwa kuanza na kipande cha Kiranjeranje - Makangaga.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**75. MHESHIMIWA DKT. ANGELINA SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ATCL itaanzisha usafiri wa Ndege kutoka Dodoma - Mwanza - Mbeya na Arusha ili kupunguza gharama kwa Wasafiri wanaokwenda Mikoa hiyo.

## WIZARA YA FEDHA:

**76. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, hatua gani zimechukuliwa kupunguza makali ya mabadiliko ya Sera za nje katika masuala ya Fedha za Maendeleo Kimataifa kwa Mataifa yaliyoendelea.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

**77. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) zinakuwa hai na zinaleta matokeo chanya kwa Taifa letu.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**78. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mkakati gani wa kujenga Viwanda vya kuchakata Chumvi Mkoani Mtwara.

**79. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Mitambo mingapi ya kutengeneza Gongo imesambazwa kwa Wananchi wanaojishughulisha na uzalishaji wa Pombe ya Gongo.

**WIZARA YA KILIMO:**

**80. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Jimbo la Singida Kaskazini utaanza.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**81. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ahadi ya ujenzi wa Mnada wa Mifugo Mngeta - Bunda.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **15 APRILI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |